



## **TAARIFA KWA UMMA KUHUSU FEDHA ZA KIMTANDAO**

Benki Kuu ya Tanzania imeshuhudia kuwepo kwa wananchi wanaotumia fedha za kimtandao (cryptocurrencies) katika kufanya malipo hapa nchini. Aidha, Benki Kuu inatambua kwamba kuna matukio ya kuhamasisha biashara ya fedha hizi za kimtandao hapa nchini ili zionekane kama ni fedha halali kwa ajili ya kufanya malipo. Vitendo hivyo ni pamoja na baadhi ya watu kudai kwamba wamewasiliana na Benki Kuu kuhusu matumizi ya fedha hizo za kimtandao.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuutahadharisha umma kwamba uuzaji, uhamasishaji wa biashara hiyo na matumizi ya fedha za kimtandao ni kinyume cha kanuni za udhibiti wa fedha za kigeni.

Benki Kuu ya Tanzania, kama taasisi pekee hapa nchini yenye mamlaka ya kuchapisha noti na kutengeneza sarafu na kuamua fedha halali kwa ajili ya matumizi hapa nchini, kama ilivyoainishwa kwenye Vifungu vya 26 na 27 vya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, inautarifu umma kwamba Shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa ajili ya kufanya malipo hapa Tanzania. Fedha zingine za kigeni zinazuzwa na taasisi zilizosajiliwa hapa nchini kwa mujibu wa taratibu zilizopo za kubadilisha fedha za kigeni. Fedha hizo zinazonunuliwa zinarudishwa kwenye nchi husika kwa mujibu taratibu zilizopo.

Hivyo, kwa taarifa hii, umma unatahadharishwa kutojikusisha na fedha za kimtandao na kwamba kufanya hivyo ni kinyume cha kanuni zilizopo za fedha za kigeni na kunaweza kusababisha hasara kwa anayehusika.

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**NOVEMBA 2019**